

MWISHO
MPYA
SANAA | SIASA | SILAHA
Hadithi Fupi
HEMA JOSEPHAT

YALIYOMO

**TABARUKU** ........ 5
**SHUKRANI** ........ 6
**UTANGULIZI** ........ 7
**SEHEMU YA KWANZA** ........ 8
**ANGANI KUNANI?** ........ 8
**SEHEMU YA PILI** ........ 12
**MCHANGA WA DHAHABU** ........ 12
**SEHEMU YA TATU** ........ 17
**MFEREJI WA MAJI** ........ 17
**SEHEMU YA NNE** ........ 21
**TAMATI YA MTUNZI** ........ 21
**SEHEMU YA TANO** ........ 30
**MWISHO MPYA** ........ 30
**HITIMISHO** ........ 38
**KUHUSU MWANDISHI** ........ 41
**KAMUSI YA MANENO** ........ 40

# MWISHO MPYA

**HEMA JOSEPHAT**

Imechapishwa na:

**Josephat Seleman Hema**

Kilimanjaro, Tanzania

Simu: +255 717 091 619

Email: josephatselemanhema@gmail.com

**© Josephat Seleman Hema**

Kava:

**Josephat Seleman Hema**

(kwa msaada wa canva.com na chatgpt)

**Toleo la Kwanza 2025**

**HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA**

## TABARUKU

Je, vijana wa kiafrika wana nafasi, uwezo na uelewa wa kuchukua hatua stahiki za kimabadiliko katika maisha yao na jamiii zao kisiasa?

Je, nini kimuandae kijana huyo kukabili changamoto za kiuongozi katika jamii yake?

Je, viongozi wako tayari kukosolewa na kusikiliza maoni yanayopinga mienendo yao kiuongozi?

Je, vijana jeuri waliosemwa na Mwalimu Nyerere waweje? Je, tunao?

Je, Sanaa inaweza kutumika kama silaha ya kisiasa?

Na Je, haya yote yana umuhimu sana katika maisha ya kijana au ni kukimbiza upepo tu?

# SHUKRANI

Shukrani kwa rafiki zangu waliopata nafasi ya kukipitia kijitabu hiki na kunipa mrejesho wa marekebisho kadha wa kadha.

## UTANGULIZI

Fadhili, kijana mdogo anatamani kuwa chachu ya mabadiliko katika jamii yake yenye changamoto chungu nzima. Anatumia ufundi wake kiuandishi kufikisha ujumbe kwenye jamii na anajikuta matatani.

Je, atarudi nyuma na kutupa taulo? Vipi kuhusu ndoto zake kubwa maishani na msichana anayempenda?

Kipi kitolewe sadaka?

## SEHEMU YA KWANZA
## ANGANI KUNANI?

Angani je, kuna nini? Mbona sifa zimezidi?
Zaidi ya huku chini, kuna nini cha zaidi?
Embu nifahamisheni, ma'na sasa imebidi,
Habari hizi nipeni, Kufahamu sina budi.

Na wewe bwana *Eloni*, mbona unatapatapa?
Kuna shida gani chini, mbona wataka kuhepa?
Maazi na Duniani, wapi heri na fanaka?
Huko tunafata nini, tusichokipata hapa?

Hapa chini duniani, kuna pambo nimepata,
Sio ndege wa mtini, sio kanga wala bata,
Tausi rangi makini, machoni ameremeta,
Nyie paeni angani, mnikute hapa hapa.

Huku akisema maneno haya kwa uthabiti, Fadhili alikatisha kauli yake baada ya kushtushwa na vumbi kuu lilioambatana na sauti ya gari likimbialo kwa kasi kuelekea upande ambao yeye na Tausi wamesimama. Wote waliduwaa kutazama, Karandinga hilo jeusi linapotokea, likiwa na maneno makubwa meupe katika ubavu wake wa kushoto yaliyoandikwa **"POLISI".**

********

"Wewe ni mshairi mzuri sana", aliongea Tausi taratibu na kwa madaha. Sautiye mfano wa ndege chiriku mwenye furaha ilizitekenya ngoma za masikio ya Fadhili na kuzisisimua. Fadhili alitabasamu na kumuangalia usoni Tausi aliyekuwa akitabasamu pia huku uso wake uking'ara mithili ya mwanga ang'avu wa Jua baada ya mvua ya radi na dhoruba kali. Mwanadada huyu mrembo wa sura, umbile na moyo alikua sehemu kubwa ya maisha ya Fadhili.

Fadhili hakuwa na rafiki mwingine wa karibu katika maisha yake zaidi ya Tausi hata akiwa na umri huu wa miaka 25. Waliishi jirani na kukua pamoja katika mtaa wa Sokoni katika mji wa Amani. Walicheza pamoja mchangani na matopeni, waliimba pamoja, walisoma pamoja na wakakua wakiona maisha ya hali moja kati yao. Hata sasa walikuwa pamoja baada ya miaka mingi kupita iliyobadilisha mambo mengi. Fadhili alikuwa mwenye haiba ya aibu, hakuweza kumtazama msichana yeyote machoni kwa sekunde zaidi ya tano. Ndio sababu hakuwa na rafiki mwingine zaidi ya Tausi. Pamoja na umri huo bado alikua na aibu hizo hasa hasa kwa wanawake. Sauti yake ya upole yenye kukwaruza kiasi iliashiria unyenyekevu na utaratibu. Lakini si kwa kila kitu. Fadhili hakuwa mpole wala mtaratibu palipo na uvunjifu wa haki. Tangu akiwa mdogo alifahamika kwa kuwa mtetezi wa wanaoonewa.

Aliamua ugomvi baina ya rafiki na kuwapatanisha. Tabia hii ilimjengea sifa njema shuleni na nyumbani hata akawa kiongozi wa wanafunzi wote alipokuwa shule ya Msingi. Nyota njema ionekanayo asubuhi ilionekana mapema sana katika maisha ya Fadhili. Alichaguliwa kujiunga na masomo ya Upili katika shule mashuhuri ya wavulana ya mkoa ulio Mashariki mwa nchi. Baada ya miaka minne ya awali, Fadhili alichaguliwa tena kuendelea na masomo ya juu ya Upili katika shule hiyo hiyo kwa miaka miwili zaidi. Alichagua masomo ya Fizikia, Kemia na Baiolojia (Elimu viumbe) akiwa na lengo la kuwa Tabibu siku za usoni. Kipindi hiki ndipo Tabibu wa mfumo wa fahamu kutoka Marekani ajulikanaye kwa jina la *Benjamin Carson* alikuwa na umaarufu sana baina ya vijana wengi weusi hasa wa bara la Afrika. Fadhili alipata kusoma kitabu kiitwacho *Gifted Hands* (Mikono Iliyobarikiwa) cha Benjamin Carson na akahamasika kuchagua mchepuo wa Sayansi kwani aliona kuwa Daktari ni njia nzuri ya kugusa maisha ya watu waliokosa matumaini. Bahati ya mtende haikumuacha Fadhili kwani alifanikiwa kupata nafasi ya kuendelea na masomo katika chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi. Hapa ni baada ya kumaliza mafunzo maalum ya kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo Fadhili alianza kupoteza msisimko wa ndoto hiyo ya Utabibu taratibu tangu akiwa mwanafunzi wa mchepuo wa sayansi. Damu yake ilianza kuchemka vuguvugu la mapinduzi ya kififikra na kimfumo katika

siasa za nchi. Kila alipokuwa akitazama yanayoendelea alikosa hamu ya kukaa shuleni na kusoma vitabu vyenye mifumo ya ndani ya mwili wa binadamu huku mifumo ya nje ikiharibiwa na siasa chafu. Hili ndilo lilomfanya aanze kushiriki katika harakati za siasa alipokuwa mwanafunzi wa chuo kikuu. Katika kipindi chote hiki, Tausi alikuwa bega kwa bega na Fadhili. Binti huyu mwenye upendo wa dhati alipata nafasi ya kusoma huko Kisimiri mkoani Arusha. Yeye alisomea mchepuo wenye masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati. Kisha akapangiwa mafunzo ya Jeshi pia na baadaye akapata nafasi katika chuo kikuu ili kusomea Uhandisi wa Kemikali. Miaka kadhaa kati yao ilikua ni kama karne nzima. Baada ya muda walikuja kugundua kuwa kati yao hakuna anayeweza kuishi bila mwenzake. Wakati Tausi anakua na kupevuka na kuwa binti mrembo mwenye rangi nyeusi ya kuvutia ya ngozi, umbo lijulikanalo kama namba nane na sauti nyororo; Fadhili alikuwa mrefu kama ngongoti, mweupe wa rangi ya ngozi kuliko Tausi, na mwembaba kama aliyekosa virutubisho muhimu vya mwili. Pamoja na utofauti huo wa kimuonekano bado walikuwa na mvuto mkubwa wawapo pamoja kiasi cha watu kuwaita mapacha. Walirandana kwa mambo mengi na damu zao zilipatana haswa.

# SEHEMU YA PILI
# MCHANGA WA DHAHABU

## MCHANGA WA DHAHABU

Salamu muhasibu, kazi yako natambua,
Jua shuruba na tabu, hata mimi nazijua,
Kazi inakusulubu, pia una familia,
Mambo mengi yakusibu, pole ninakupatia.

Wengi wamekuwa bubu, kwako nimeshasogea,
Najua waweza jibu, maswali nakuletea,
Haya yanayotusibu, hata wewe hukujua?
Eti mchanga dhahabu, mwingi umeshapotea.

Ule mkataba bubu, nawe hukuupitia?
Vipi na makatibu, nao hawakuujua,
Waziri ameshatubu, pengine alisinzia.
Japo tumeshaharibu, kisa ni makinikia.

Fadhili alifikia uamuzi mgumu wa kusimamisha masomo kwa muda wa mwaka mmoja kwa kigezo cha kupata muda wa kutuliza akili akiwa mwaka wa nne wa masomo ya Udaktari. Alikuwa ameshakereka sana na uendeshaji wa miradi ya jimbo la Amani iliyojaa dhuluma, rushwa na uonevu wa kila hali

kwa watu wa kipato cha chini. Hii ni baada ya kaka yake mkubwa kubambikiwa kesi ya wizi wa madini katika mgodi wa dhahabu alipokuwa akifanya kazi kama mlinzi. Japo hili lilimuumiza sana Fadhili hasa baada ya kung'amua kiundani kuwa kaka yake alikuwa akitekeleza majukumu yake ya kazi, yaani kulinda usafirishaji wa madini kwa mustakabali wa uchumi wa Taifa na watu wake waliokuwa wakiganga njaa kwa hali na mali katika mgodi huo, wakijichosha kwa kazi ngumu yenye ujira hafifu. Fadhili akaazimia kurudi nyumbani kutafuta haki kwa ajili ya kaka yake na wananchi wa jimbo hilo waliokuwa na nafasi kubwa kwenye moyo wake.

Hapa ndipo Fadhili alipoamua kujiunga rasmi kwenye siasa akiwa na lengo la kuondoa uongozi badhirifu uliokosa mipango ya uwajibikaji katika ofisi za serikali jimboni kwake. Fadhili alitumia vyema kipaji chake cha uandishi wa mashairi ili kuwasilisha mawazo yake na kupaza sauti ya jamii yake. Baada ya kupata nafasi katika gazeti binafsi la NURU GIZANI aliandika shairi lenye kichwa kisemacho “MCHANGA WA DHAHABU” lililogusia usafirishaji haramu wa mchanga katika mgodi wa dhahabu jimboni kwake na kwa namna viongozi wa juu hasa Mbunge walivyokuwa wakitumia mwanya huu kuiba madini na kujilimbikizia mali ilihali wachimbaji wakikosa malipo kwa kigezo cha upatikanaji hafifu wa madini. Hapa ndipo alipoanza kupokea vitisho kutoka kwa watu wasiojulikana lakini hakuogopa wala kufa moyo.

Shairi la "TAMATI YA MTUNZI" lilifuata likielezea namna yeye kama mwandishi na mtetezi wa haki za wanyonge anavyoonekana katika jamii iliyojaa ufisadi. Wakati wananchi wa hali ya chini wakimsifu na kumuona shujaa na mkombozi, viongozi wanaonufaika na mfumo huo kandamizi walimuona tishio kwa maslahi yao.

Tausi alimuona Fadhili katika taswira tofauti tofauti na njema, lakini mara ghafla alishikwa na hofu baada ya kujua kuwa Fadhili alianza kupokea vitisho vya usalama wa maisha yake. Asubuhi hii tulivu, ikiwa ni siku mojawapo ya likizo ya kimasomo kwa Tausi walipanga wakutane katika uwanda wa Amani kama walivyouita. Tausi alimuomba Fadhili wakutane mahali hapo ambapo paliwakutanisha wakiwa watoto wadogo. Sehemu hiyo iliyo karibu na shamba kubwa la Pamba; mali ya wananchi wajasiriamali wa mtaa huo pia ilikua na visima maarufu vya maji yasiyokauka. Uwanda wa Amani ilikua ni sehemu yenye kilima kidogo kinachompa mtu nafasi ya kuona sehemu kubwa ya mji wa Amani kutoka upande huo wa Mashariki.

Tausi na Fadhili walikutana mahali hapa mara kwa mara kwa maongezi yanayohitaji utulivu wa fikra. Pamoja na maongezi pia walipata muda wa kusoma mashairi mbalimbali ambayo Fadhili amekuwa akiyaandika kwa muda mrefu sasa katika kitabu chake cha Ushairi. Tausi alikuja na matoleo mawili ya gazeti la NURU GIZANI na Fadhili alikuja na kitabu chake cha

ushairi alichokiita NJOZI NJEMA. Huku upepo mwanana ukiwapepea, Fadhili alisoma mashairi mawili mazuri aliyoyaandika kwa ajili ya Tausi aliyekuwa akiyasikiliza kwa makini huku usoni akiwa amejaa Tabasamu maridhawa. Shairi la “ANGANI KUNANI?” lilikuwa la kufurahisha likielezea namna ambayo ndege Tausi anavyoishi nchi kavu na jinsi Fadhili asivyoona haja ya kwenda angani kwa sababu Tausi yu nchi kavu. NURU YA MILELE lilielezea namna urafiki wa Fadhili na Tausi ulivyodumu na kuwa msaada mkubwa kwao wote mpaka leo, lilimalizia na fikra ya kuhuzunisha kuhusu wakati ujao pasipo mmoja kati yao. Tausi alitokwa na machozi kusikiliza sehemu hiyo ya ushairi iliyosema;

Na daima itang’ara, siku mbali ukienda,
Hata uvuke mabara, miaka kumi na kenda,
N’takuwaza kila mara, sitasahau uwanda,
Nitajawa na subira, sitakoma kukupenda.

Akiwa ameegemea begani kwa Fadhili alimshika mkono wake mmoja kwa mikono yake yote miwili na kumnong'oneza, "Ninakupenda sana Fadhili". Pasipo Fadhili kusema kitu, Tausi alisikika tena akisema, "Wewe ni mshairi mzuri sana", aliongea Tausi wakati huu taratibu na kwa madaha. Sautiye mfano wa ndege chiriku mwenye furaha ilizigusa ngoma za masikio ya Fadhili na kuzisisimua. Fadhili alitabasamu na kumuangalia usoni Tausi

ambaye sasa alikuwa akitabasamu pia huku uso wake uking'ara mithili ya mwanga ang'avu wa Jua baada ya mvua ya radi na dhoruba kali.

# SEHEMU YA TATU
# MFEREJI WA MAJI

## MFEREJI WA MAJI

Ule mto wa neema, katikati ya kijiji,
Wenye wingi wa neema, daima twauhitaji,
Mto umejaa mema, ni matamu yake maji,
Mbona sasa unakwama, huku kwetu hauji?

Siku sasa zayoyoma, tumepungukiwa maji,
Serikali wanasema, tatizo ni la kijiji,
Eti miti tunachoma, tukitafuta mitaji,
Hili linatupa homa, bora kingine kipaji.

Ila watu wanasema, kumezuka mfereji,
Wajanja walishapima, katikati ya kijiji,
Hapo mali wanachuma, kiwe chanzo cha ulaji,
Sie namba tunasoma, wao wanajifariji.

Viongozi wamezima, huku maji yanaisha,
Hata tunapolalama, wanasema tunachosha,
Tumekosa pa kusema, tumebaki sikitisha,
Hata kama tukisema, tamaa watukatisha.

Tunataka mtaalamu, wa kufanya utafiti,
Mfereji wa hujumu, inapaswa kudhibiti,
Hili swala la muhimu, tuukomboe wakati,
Lisije likawa sumu, tukakosa uthabiti.

Fadhili hali asijue ni jawabu lipi lingelifaa zaidi kusema alifunga kitabu chake na kuangalia upande unaotazamana na mji wa Amani. Alizama katika lindi kuu la mawazo yaliyochanganyikana na hofu, woga, huruma, hasira, furaha na mwisho mwema kwa habari ya mapambano ya kutafuta haki na usawa. Tausi hali akiangalia chini alisema kwa sauti yenye kuashiria hofu ba mashaka.

"Wakati mwingine natamani nikuambie ukache mambo ya siasa. Napenda sana mashairi yako yenye dhima za Upendo, Amani na Utunzaji wa Mazingira", alisita kidogo kisha akaendelea,

"Napenda pia na mengineyo, lakini yanakuweka kwenye wakati mgumu sana kiasi ninajawa na hofu kuu wakati mwingine".

Kimya kilitawala,Tausi akipekua kurasa za magazeti aliyokuwa nayo mkononi na kutazama mashairi mawili maarufu ya Fadhili, "MCHANGA WA DHAHABU" na "TAMATI YA MTUNZI". Yaliandikwa kwa ustadi wa hali ya juu na kuleta mvuto kwa msomaji, lakini umahiri huo ndio ulikuwa umemtia

Fadhili matatani ambaye pamoja na kuwa salama alikuwa amekwishanusa harufu ya hatari mpaka muda huo. Kukiwa kumegubikwa na ukimya, ilhali kila mmoja akiwa amezama kwenye rindi la fikra anuwai, ilisikika sauti ya muungurumo wa gari kuelekea upande ambao Fadhili na Tausi wamekaa. Sauti hii ilizusha udadisi wa ghafla na kumshtua Fadhili aliyeinuka ghafla na kutazama upande sauti hiyo ilipokuwa inatokea. Akahamaki kwa sauti ya kunong'ona,

"Mungu wangu, wamepajuaje huku?”.

Tausi alijiunga katika hamaki hiyo, akijibanza nyuma ya Fadhili,

"Mtume!”

Tausi alishtuka sauti ikimtoka. Wakati Karandinga jeusi lenye maandishi makubwa **"POLISI"** katika ubavu wake wa kushoto likisonga kuelekea waliposimama Tausi na Fadhili, Fadhili alimkabidhi Tausi kitabu chake cha ushairi huku akimnong'oneza,

"Tunza kitabu hiki, ni zawadi yako. Uje nacho mahali hapa muda kama huu kesho tafadhali usiache", wakati Tausi akihamaki kitabu kilidondoka chini asijue la kufanya, gari lilisimama mbele yao na askari wawili walishuka kuelekea alipo Fadhili.

"Uko chini ya ulinzi kuanzia sasa, utapata maelezo mengine kituoni", Askari mmoja mrefu mwenye sura iliyojaa jeuri na majivuno alizungumza akimtazama Fadhili usoni huku akitabasamu na kuifungua pingu iliyokuwa mikononi mwake akijiandaa kumfunga Fadhili.

Tausi akitetemeka kwa woga ilhali kitabu kikiwa chini huku magazeti mawili yaliyokuwa mahali walipokaa yakipeperushwa na upepo uliovuma kwa kasi. Ndani ya dakika mbili Fadhili alikuwa ametiwa pingu na kusekwa ndani ya gari la Polisi.

Siku hii ilianza kwa namna hii.

********

Askari hawa hawakuzungumza chochote wakati gari hili likikatiza mitaa mpaka kwenye kituo cha Polisi kilicho upande mwingine wa mji wa Amani. Ilichukua kama dakika kumi na tano kufika na kumkabidhi Fadhili katika dawati la mapokezi katika kituo cha Polisi. Fadhili aliyetazamwa kama kijana mdogo aliyekosa muelekeo mwema wa maisha alisekwa ndani ya chumba kidogo cha mahabusu baada ya kukabidhi mali zake kama simu na fedha pale mapokezi. Juhudi zake za kulalamika na kuuliza kwanini haya yanamtokea hazikuzaa matunda hasa baada ya chumba cha mahabusu kufungwa, kiza kutawala pasipo kusikia kauli yoyote kutoka kwa askari hao.

## SEHEMU YA NNE
## TAMATI YA MTUNZI

TAMATI YA MTUNZI

Laiti ningalijua, kutunga japo utenzi,
Sifa ningemwagia, japo wengi wamuenzi,
Sana ningemsifia, alivyokuwa kipenzi,
Daima nitaililia, tamati yake mtunzi.

Pale alipoishia, alionesha ujuzi,
Kalamu akaachia, ilipomwishia pumzi,
Huku tukimwangalia, ilo bora yake kazi,
Wote tuliobakia, kumuiga hatuwezi.

Yale maneno sawia, aliyoyaweka wazi,
Wino katuandikia, kwa ukweli na uwazi,
Fahamu kutufungua, maarifa waziwazi,
Bado tunakumbukia, hayatuishi majonzi.

Kichwa busara sawia, alikua na makuzi,
Hata anayoongea, yamejaa uchunguzi,
Makini anang’amua, ni kama mpelelezi,
Zile siri azojua, ni za hatari baadhi.

Mioyo aliinua, kwa makala changanuzi,
Tumaini alitoa, kwa vizazi na vizazi,
Alitembea dunia, na kutoa fafanuzi,
Wale wanaokimbia, yanawatoka machozi.

Japo bado apumua, alishaiacha kazi,
Anasema ina*bore*, yamnyima usingizi,
Vitisho anapokea, awekapo mambo wazi,
Kaona kujiokoa, aache upaparazi.

Muwazi anapokua, kuna watu awaudhi,
Wako nyuma ya pazia, wanaleta vizuizi,
Vigogo akiumbua, aharibu yao kazi,
Hapo kilichofatia, ni tamati ya mtunzi.

Hali akiwa katika lindi la mawazo yenye mchanganyiko wa maswali lukuki na hasira, Fadhili aliyeiona siku hii katika mawazo yake hapo kabla, alishtushwa na sauti kuu ya msukumo wa mlango wa chumba hicho cha mahabusu ukifunguliwa. Hii ilikuwa baada ya kitambo kirefu kidogo kupita. Aliingia mtu mmoja mrefu wa makamo mwenye sare za askari magereza na nyota mbili begani mwake. Mtu huyu mwenye haiba ya ukatiri na sura yenye mikunyo ya hasira alisindikizwa na askari mwingine aliyekuwa amebeba kiti cha

chuma alichokiweka kama umbali wa mita moja kutoka chini alipokuwa amekaa Fadhili, kajiinamia. Yule askari mwingine aliondoka mara baada ya kuweka kiti kile chini akiuacha mlango ukiwa na uwazi kidogo uliopitisha mwanga hafifu na hewa. Baada ya kuketi na kumtazama Fadhili kwa makini, Askari huyu aliyekuwa na jina lililosomeka “Luteni Majaliwa” katika pande wa kushoto kifuani wa sare yake nadhifu, alitabasamu kwa dharau na kusema,

"Tabibu Mwandishi, Mwana harakati, Mkombozi, Nelson Mandela wa kizazi kipya",

Alimalizia kwa kuangua kicheko kidogo cha dharau huku sauti yake yenye mikwaruzo ikitoka na kubugudhi ngoma za masikio ya Fadhili.

"Unajua unachofanya?",

Aliingiza mkono katika mfuko wake na kutoa kipande kidogo cha gazeti kilichokatwa na kuacha shemu ndogo yenye shairi la "MWISHO MPYA" aliloliandika Fadhili kwa ajili ya toleo jipya la gazeti la NURU GIZANI la siku hiyo. Shairi hili liligusia matumaini mapya ya maisha bora kwa wananchi wa jimbo la Amani ikiwa watachagua viongozi waadilifu katika uchaguzi mkuu wa mwakani. Pasi na kusubiri majibu kutoka kwa Fadhili aliongeza,

"Unaharibu *future yako",* akavuta pumzi kidogo na kuendelea,

"Ningelikushauri uzingatie elimu yako ya utabibu, au uandishi wa Riwaya na Mashairi ya Mapenzi, na siyo huu upuuzi unaofanya, Itaku*cost*",

Alisimama na kumsogelea Fadhili na kumwambia,

"Hujaguswa mpaka sasa, una bahati sana. Nitakupa nafasi nyingine ya kuamua hatima ya maisha yako",

Alisema na kuondoka taratibu katika chumba hicho akiacha mlango wazi. Haikupita dakika mbili alirudi akiwa na karatasi mbili zilizochapwa maelezo kurasa zote nne. Alizikunja na kuonesha sehemu ya mwisho iliyokuwa na jina la FADHILI MTOKAMBALI na kijisehemu chenye mstari wa vinukta na neno “sahihi” chini yake katika mabano. Askari huyu aliweka karatasi hii juu ya sehemu ya kukalia ya kiti kilichokuwa kitupu kwa wakati huo na kutoa kalamu katika mfuko wake wa shati kisha kuielekeza kwa Fadhili huku akisema,

"Tia sahihi yako hapa uende nyumbani, mahali hapa sio pazuri kwa kijana msomi kama wewe. Utokapo hapa ukajiandae kurudi chuoni na kamwe usijihusishe tena na masuala ya siasa za Ukombozi",

Alimaliza huku macho yake yakianza kumtoka kwa hasira baada ya kuona Fadhili akimtazama tu pasipo kuonesha muitikio wowote. Akaongeza,

”Lakini, Natamani sana nikuelewe zaidi. Kwa maneno machache sana unaweza sema unataka nini?”

Fadhili hakusema chochote, Kapteni Majaliwa akaendelea.

“Wanasema mkosoaji anaijua njia lakini hajui kuendesha gari. Wewe bado ni kijana mdogo sana, chukua muda kujifunza mifumo inavyofanya kazi. Achana na *naivity of youth*. Soma mabuku, pata ujuzi, tengeneza pesa na fursa, safiri na pia *fall in love*. Hapo ndipo utakapojua zaidi unataka nini na wigo wa uwezo na upeo wako kubadilisha mambo. Sasa hivi nashindwa kukuchukulia *serious* sana. Hakuna kitu *substantial* umefanya na hauijui *kwanini* yako”, Akaonesha ishara ya kumpa kalamu Fadhili.

"Siwezi kutia sahihi yangu pasipo kusoma nyaraka hiyo", Fadhili alijibu kwa upole huku Askari huyu akikenua kwa hasira na uchungu.

"Msomi Hahaha", Askari Alijichekelesha na kuendelea.

"Unaweza kukaa humu mpaka huko nje wakakusahau. Lakini pia haujaonja pigo hata moja, nadhani ndio sababu unahisi uko *vacation* humu sio?”

Alivuta pumzi kwa hasira na kuongezea tena. "Nakupa nafasi ya mwish...” Alisema na kukatishwa na sauti thabiti ya Fadhili.

"Sitatia saini mpaka niisome karatasi hiyo Afande, ni haki yangu", Fadhili alijibu huku akimtazama usoni.

"Unataka haki sio? Sawa sawa", Askari alimjibu huku akirudisha kalamu mfukoni na kuikunja karatasi ile, akitabasamu kwa kebehi.

Alitoka nje ya chumba hicho na kusikika akitoa maagizo kadhaa kwa Askari mwingine nje ya chumba hicho. Mara ghafla mlango ukafungwa na giza totoro likakitawala chumba hicho tena. Hali akiwa amejawa na hasira, Fadhili alikumbuka kuwa hajapata kutia kitu tumboni mpaka wakati huo. Japo hakuwa na saa na hakujua majira, uwepo wa kelele za mbu ulimjulisha kuwa ilikua mwanzo wa usiku na hakuwa akisikia njaa wala hamu ya kula kabisa kutokana na hasira.

"Hata hivyo…", Fadhili aliwaza. "Siwezi kuendelea kukaa katika hali hii. Pindi kutakapokucha nitaondoka mahali hapa",

Alijisemea akiinuka na kuelekea mahali mlango wa chumba hicho cha mahabusu ulipo. Aliposogea na kuushikilia mlango huo akikusanya nguvu zote kuufungua kwa kuvunja kufuli lilichokuwepo kwa nje. Alifumba macho na kuuma midomo yake ya chini kwa hasira na kupania. Mara ghafla akiwa hana hili wala lile, mlango ulisukumwa kwa kasi kutoka nje na kupiga paji

lake la uso kwa nguvu, kisha kumtupa nyuma kwa kasi. Akajikuta akiangukia ukuta aliokuwa ameuegemea hapo awali. Maumivu makali kutoka sehemu ya nyuma ya kichwa na mgongo yalianza kupanda ghafla huku giza lenye nyota nyota ndogo likianza kutanda katika macho yake. Hali ya umajimaji katika paji lake la uso ikiambatana na maumivu makali kama ya wembe mkali ukatavyo ilimlazimu asogeze kiganja chake cha mkono wa kulia na kuchovya sehemu ya maji hayo ili kuitazama rangiye. Hali yake haikumuwezesha kutambua rangi ya majimaji hayo kwani giza kuu lilizizidi nguvu mboni za macho na kope nzito zilifunika macho yake kwa utulivu huku mwili hafifu ulioishiwa nguvu ukijibwaga chini taratibu.

*********

Tausi alikesha akibubujikwa na machozi huku akiwa amekikumbatia kitabu cha Fadhili. Upweke mkuu na huzuni vilimshinda nguvu japokuwa haikuwa mara ya kwanza kuwa mbali na Fadhili, lakini haijawahi kuwa kwa hali ile. Alihofia usalama na hasa maisha ya Fadhili ambaye ndiye kila kitu kwake. Kulikuwa na habari mbili tatu za kitambo kuhusu waandishi mbalimbali na wanaharakati wa haki na usawa waliopotea katika mazingira yenye kutatanisha siku za nyuma na hawakuonekana tena. Hali hii ilimtisha, hakutaka kudhani kuwa Fadhili alikuwa akielekea katika hali hiyo. Tausi hakumjuza mtu yoyote kuhusu tukio lile mpaka muda huo. Ni yeye aliyepewa

taarifa na mama yake Fadhili kuhusu Fadhili kushikiliwa kituo cha Polisi kwa kesi ya uchochezi na upotoshaji kupitia Magazeti. Ndugu zake waliamua kwenda kituo cha Polisi lakini hawakuruhusiwa kuingia na wakaambiwa waende siku inayofuata hivyo Tausi alijipanga kuwa mmoja wao. Usiku huu Tausi, kwa mara ya kwanza, aliandika shairi mahususi kwa ajili ya Fadhili na alipanga kumpatia Fadhili alisome muda watakapokutana tena.

Kulipoanza kupambazuka Tausi alikumbuka maneno ya Fadhili, “Tunza kitabu hiki, ni zawadi yako. Uje nacho mahali hapa muda kama huu kesho tafadhali usiache". Alijikurupusha na kutazama saa ya ukutani iliyoonesha muda wa saa 12 kasorobo alfajiri. Aliamua kuvaa nguo zitakazomkinga na baridi ya alfajiri ile na kuondoka kwa tahadhari huku akiwa na kitabu cha Fadhili kifuani mwake, akikikumbatia kwa mikono miwili. Alipita nyuma ya nyumba kulikokuwa na vichochoro kadhaa na sauti za watu wakiamka na kujiandaa na shughuli za siku mpya. Hakukua na watu wengi na kiza cha alfajiri kilikuwa bado kingali walau kimetamalaki. Tausi alitembea kwa haraka pasipo kusemezana na mtu yoyote hali sura yake ameificha na kofia ya sweta lake kubwa jeusi. Hatua kadhaa mbele alifuata njia ya mashambani kuelekea mahali husika ambapo alifika muda wa saa 12 na nusu alfajiri ikiwa ni masaa mawili kabla ya muda ambao Fadhili alimuagiza awepo.

Hali akiwa na kukata tamaa kumuona Fadhili tena mahali hapo siku za usoni, Tausi alijisemea. "Fadhili, nitashinda mahali hapa siku ya leo, nitasoma mashairi yako na kuyaimba,pia nitakuombea. Uwe salama Fadhili wangu, tutaonana muda si mrefu tukifurahi na kuimba nyimbo za ushindi.....", ghafla alisita baada ya kusikia sauti kama ya mnyama mdogo aliyejibanza katika kichaka kidogo akijitikisa taratibu. Alikaa kimya kidogo ili kuhakikisha kama kweli aliisikia sauti hiyo iliyokuwa inatokea nyuma yake. Mapigo ya moyo wake yalianza kukimbia kwa kasi hasa baada ya kusikia sauti ya mtu avutaye pumzi kwa ghadhabu. Asijue la kufanya alianza kugeuka nyuma taratibu na kwa tahadhari kubwa.

## SEHEMU YA TANO
## MWISHO MPYA

MWISHO MPYA

Afrika Afrika, tega sikio sikia,
Nakuita Afrika, kitu ninaulizia,
Ni lini tutafika, nasi tukafurahia,
Kwenye nchi ya baraka, lini tutashangilia?

Afrika Afrika, mwanzo ulitulemea,
Tulinyonywa tukachoka, nguvu zikatuishia,
Japo siku ilifika, wenyewe tukabakia,
Dola sisi tukashika, Imani ikaingia.

Afrika Afrika, bado tu kutengemaa?
Hatima tunayotaka, ni kama imekawia,
Mbona hofu na mashaka, bado vinatulemea?
Mwisho mpya tunataka, sio huu nakwambia.

"Bado unapumua? Nikajua nimefanya pasipo kukusudia shughuli inayotakiwa kufanyika mapema asubuhi", alizungumza kwa hofu kuu Askari aliyekuwa ameinama kumtazama Fadhili aliyekuwa akifungua macho

taratibu huku akigugumia kwa maumivu makali ambayo sasa yalikuwa yakiukata mwili mzima uliokuwa na uchovu mkuu.

"Niliagizwa nikuletee chakula hiki, lakini nakushauri kamwe usikitie kinywani mwako", alizungumza akionesha kisanduku kidogo cha chakula kilichokuwa pembeni ya Fadhili na chupa ndogo ya maji ya kunywa. Fadhili akiwa ameduwaa asijue la kufanya alimtazama usoni askari yule ambaye ndiye yule yule aliyekuwa pamoja na Luteni Majaliwa hapo awali lakini sasa alizungumza maneno kama si mmoja wa kundi hilo la askari ambao walianza kumuingiza rasmi kwenye lindi la mateso. Mara ghafla akang'amua kuwa sura hii si ngeni machoni mwake, lakini kumbukumbu sahihi zilimtupa mkono. "Unaweza kusimama?" askari huyo aliingiza mkono chini ya bega la Fadhili na kumuinua Fadhili ambaye ghafla nguvu mpya zilianza kumjia, akajikakamua na kusimama ilihali mkono mmoja ukiwa umeshikilia ukuta wa chumba hicho.

"Nifuate", aliagiza askari huyo kwa sauti yenye tahadhari na kuanza kuongoza njia kuelekea mlangoni, akaufungua mlango ili Fadhili apite kwanza kuelekea nje ya chumba hicho ambako giza totoro na baridi kali vilikuwa na muunganiko maridhawa.

"Sasa ni saa ngapi?" Fadhili aliuliza huku akijikongoja kumfuata askari aliyekuwa akitembea kwa tahadhari ambaye ghafla aligeuka na kutumia vidole vyake kumuonesha Fadhili ishara ya kufunga kinywa chake. Pamoja, walifuata korido pweke na kuingia katika chumba kilichokuwa wazi na makorokoro mengi, askari yule alitoa baadhi ya vitu vilivyokuwa vimerundikana upande mmoja wa kuta za chumba hicho ndipo ghafla pakajitokeza kitundu kidogo katika ukuta huo, askari akageuka kumtazama Fadhili na kumwambia. "Kimbia uokoe maisha yako, pita hapa na usitazame nyuma wala kusitasita, mimi nitajua la kufanya huku mara utakapoondoka, haya hima". Fadhili hakujiuliza mara mbili, akili yake na mwili vilifyatuka ghafla akajipenyeza katika kitundu hicho huku akihema kwa haraka haraka. "Kila la heri *right marker*", askari yule alisema huku akianza kurudishia makorokoro yale katika ukuta ule wakati Fadhili akitokomea.

"Fikirini!" Fadhili alihamaki wakati akimalizia kutoka "Kimbia, Kimbia, pamekaribia kukucha", Askari yule alinong'ona huku akiendelea kushindilia makorokoro yale, sauti ambayo Fadhili aliisikia kama mwangi wa tahadhari utokao mbali. Mbele yake kulikua na pori pweke. Fadhili alishika njia na kutokomea kwa kasi na tahadhari asijue hatima yake na matokeo ya hiki akifanyacho.

“Unakimbia nini?”, Sauti ilisikika ikimuuliza katikati ya pori hili asijue inatokea wapi. Sauti hii haikuwa ngeni masikioni mwake. Fadhili alishtuka akajikwaa na kudondoka chini.

“Kimbiaaaa !”, Sauti ile ile iliamrisha kwa mamlaka. Fadhili alijikusanya na kufyatuka kama risasi hali akijiuliza ni wapi sauti ile ilikuwa inatokea. Ghafla akang’amua fika sauti ile inapotokea huku ikiendelea kumsemesha hali akikaza mwendo.

“Unatafuta nini zaidi, Unataka nini hasa wewe? Una uhakika utakipata? *Ndege mjanja hunaswa na tundu bovu*.” Sauti iliendelea Fadhili akiitafakari na kwa mara ya kwanza wazo hili la “Unataka nini” likampa mzigo mzito moyoni na akilini. Sauti hii iliyokuwa ikitoka kuchwani mwake ilikoma kumpa muda kufikiria. Ilikuwa ni sauti yake. Sauti ya Fadhili.

“Nataka nini mimi, mbona ni kama vile sina jawabu mujarabu?” Fadhili akawaza huku akiendelea kukimbia.

Haikuzidi nusu saa Fadhili aliyatambua mazingira aliyokuwepo, palikuwa ni upande wa pili wa maeneo ya kituo cha Polisi ambako kulikua na mashamba ya kanisa kubwa mjini Amani, hivyo akajua ni njia ipi salama ya kutumia kufika aendako. Lakini aende wapi? Akili yake ikamtuma kuelekea katika bustani ya Amani hivyo akashika njia moja kwa moja, akichanja mbuga

katikati ya kiza na baridi huku mwanga mpya wa siku ukianza kuangaza kwa mbali na yeye akikaribia kuufikia uwanda wa Amani, ndipo alipojua kuwa alipoteza fahamu kwa zaidi ya masaa saba usiku uliopita. Alijibwaga katika kichaka karibu na sehemu wakaapo yeye na Tausi, akatulia tuli akisikilizia maumivu mpaka aliposikia sauti ya mtu akijongea mahali pale na kuanza kulitaja jina lake. Sauti ya Tausi ndio ikamtoa kichakani.

"Fadhili!", Tausi alihamaki akiweka kitabu chini na kumkimbilia Fadhili aliyekuwa na damu iliyoganda katika paji la uso,vumbi jingi miguuni, harufu kali katika nguo zake, maumivu, uchovu na njaa kali sana. Masaa machache yalitosha kubadilisha vitu vingi kwake.

"Nini kimetokea? wamekutesa?", Tausi aliuliza akiwa amemkumbatia Fadhili aliyekuwa akipepesuka huku akimtazama usoni machozi yakiwadondoka wote wawili.

"Wanataka kuniangamiza, Fikirini amenitorosha", Fadhili alijibu kwa jazba.

”Nani anataka kukuangamiza? Fikirini ni nani?"

Tausi aliuliza kwa hofu kuu. Maswali ambayo Fadhili hakuyajibu. Ilikuwa ni hadithi ndefu ya kuhusu urafiki wake wake na Fikirini waliyekutana katika kambi ya mafunzo ya mara baada ya kumaliza kidato cha sita. Fadhili kutokana na urefu wake alichaguliwa kuwa kiongozi wa mstari wa kulia

katika mazoezi ya kwata, kwa lugha ya kiingereza akijulikana kama *right marker*. Hivyo ndivyo Fikirini alipendelea kumuita, wakati urafiki wao ukishamiri katika kipindi hicho cha mafunzo magumu. Hakujua kuwa rafiki yake amekuja kuwa askari baada ya mafunzo yale kwani hawakupata kuendelea kuwasiliana mara tu baada ya kumaliza muda wao wa mafunzo na kuhitimu. Sasa Fikirini ndiye aliyemuokoa kutoka katika dhahama hiyo huku asijue ni lipi linalotakiwa kufanyika haswa wakati huo, moyoni akiazimia kupambana mpaka hatua ya mwisho ifike, nayo si nyingine ila kufanikisha ukombozi wa wananchi wa jimbo lake. Akijitutumua maneno haya yakamtoka,

"Mapambano kamili yameanza, nitapambana mpaka mwisho. Sitakuwa na mwisho kama wa wanaharakati wengine, kufyata mkia na kunyamaza. Sitakuwa kama mwandishi yule katika shairi langu la TAMATI YA MTUNZI. Nitakuwa na mwisho mpya, mwisho utakaoshuhudia ushindi katika mapambano dhidi ya ufisadi. Mwisho wenye haki na usawa kwa kil........",

Huku akisema maneno haya kwa uthabiti, Fadhili alikatisha kauli yake baada ya kushtushwa na vumbi kuu lilioambatana na sauti ya gari likimbialo kwa kasi kuelekea upande ambao yeye na Tausi wamesimama. Wote waliduwaa

kutazama, Karandinga hilo jeusi linapotokea, likiwa na maneno makubwa meusi katika ubavu wake wa kushoto yaliyoandikwa "**POLISI**".

Kipande kidogo cha karatasi alichokuwa nacho Tausi mikononi mwake kilipeperushwa na upepo na vumbi huku mikono yake ikiishiwa nguvu. Kichwa cha karatasi hiyo yenye mwandiko wa Tausi kiliandikwa “WATAKA NINI MPENZI?” kikifuatiwa na maneno haya:

**WATAKA NINI MPENZI?**

Wataka nini mpenzi, sema leo nijue?
Nauliza kwa utenzi, na useme nisikie,
Nimejawa na simanzi, unanifanya nilie,
Wataka nini mpenzi, sema mi nikusikie.

Ukiyataka mapendo, kwangu yapo pindukia,
Ni churudu si ndondondo, yafurika kuvamia,
Nina *unlimited bundle*, yajaa kumwagikia,
Vigelegele vishindo, nakupenda kuzimia.

Ukiitaka amani, utulivu nayo haki,

Kwangu tulia moyoni, hakikisha hautoki,

Barizi kibarazani, bila mikikimikiki,

Mpenzi tulia ndani, nje hakumithiliki.

Mpenzi wataka nini, nakupenda unajua,

Wananchi ni wahuni, matapeli wa Dunia,

Hawajali kama mimi, wana zao familia,

Upendo wangu thamini, moyo wangu shikilia.

-MWISHO-

**HITIMISHO**

TANZANIA NAKUPENDA

Tanzania nakupenda, moyoni umeingia,
Hata njaa nikishinda, wapi nitakimbilia?
Uzalendo ninalinda, hata kama ninalia,
Kuna muda wanishinda, nami binadamu pia.

Kwanza nilitafakari, kwa marefu na mapana,
Jinsi ulivyo mzuri, ni kama kasoro huna,
Japo nawe una shari, ila sio nyingi sana,
Moyo ukanishauri, nyumbani kutulizana.

Tumepewa utulivu, wa miaka na miaka,
Hatujapewa makovu, sisi tulisalimika,
Wala si mengi maovu, wengi wamestaarabika,
Ila wapo na wavivu, japo wanahesabika.

Namkumbuka mwalimu, alivyotuunganisha,
Dini kabila ni sumu, sisi wamoja maisha,
Kila mtu wa muhimu, umoja kufanikisha,
Tukapata na elimu, japo mwanzo haikutosha.

Huko nje nikienda, Tanzania nitarudi,
Kuna baridi huenda, muda fulani lazidi,
Ubaguzi sitapenda, ule wa kimakusudi,
Nyumbani wananipenda, upendo ninafaidi.

Mkacha kwao mtumwa, alishasema Mwalimu,
Hili jambo linasemwa, tena mnalifahamu,
Ya nini kuwa mtumwa? nitabaki humu humu.
Hata kama nikiumwa, unazo tiba muhimu.

Sikuachi Tanzania, nasema hili kwa wazi,
Hili nimeshaamua, sibadili maamuzi,
Wale mnaokimbia, hata kwa kupiga mbizi,
Nashauri kubakia, tuzijenge zama hizi.

## KAMUSI YA MANENO

**Eloni**-*Elon Musk*, mfanyabiashara wa kimarekani mwenye asili ya Afrika kusini anayeamini katika kuanzisha maisha ya binadamu katika sayari ya Maazi.

***Fall in Love***-Kumpenda mtu, kuingia katika mahusiano ya kimapenzi naye.

**Ina*bore***-Isiyo ya kufurahisha, inayokinai kirahisi

**Itaku*cost***-Itakuletea madhara

***Naivity of Youth***-Upofu wa ujana. Kuamini katika kuleta matokeo makubwa kwenye mifumo kongwe pasipo kuwa na uwezo na fursa stahiki.

***Substantia**l*-Kitu chenye uzito mkubwa kimantiki.

***Serious***-Hali ya kuwa makini au na maana.

***Unlimited Bundle***-Kifurushi cha mtandao kisichokwisha.

***Pan-Africanism***-Nadharia ya Waafrika kujitegemea na kufanya vizuri kwenye chanja zote za kimaisha.

## KUHUSU MWANDISHI

Hema Josephat ni Mtanzania mzalendo anayeamini katika *Pan-Africanism*. Kitaalumna ni Mfamasia na amebobea kwenye utaalamu wa tafiti za kisayansi, sayansi ya data za afya, mnyororo wa ugavi na matumizi ya akili mnemba katika sekta ya afya. Kando na taaluma yake, Hema ni mwandishi wa mashairi na hadithi fupi. **Mwisho Mpya** ni kazi ya kwanza ya Hema Josephat kwa lugha ya Kiswahili.

Kazi nyingine za Hema Josephat:

**Dear Brown** (Hadithi fupi kwa lugha ya Kiingereza)

**365 Days of a Poet** (Mkusanyiko wa wa mashairi 200 kwa lugha ya Kiingereza)

**The Scapel** (Mkusanyiko wa kazi mbalimbali za Sanaa kutoka kwa wasanii tofauti tofauti kama vile michoro na mashairi kwa lugha ya Kiingereza)



Hema Josephat ni Mfamasia anayeishi na kufanya kazi na kuishi kaskazini mwa Tanzania. Hema amebobea kwenye utaalamu katika tafiti, data za afya, mnyororo wa ugavi na matumizi ya akili mnemba katika sekta ya afya. Kando na taaluma yake, Hema ni mwandishi wa mashairi na hadithi fupi.

***********

Fadhili Mtokambali akiwa mwanafunzi wa masomo ya utabibu anaamua kushiriki katika harakati za kutetea haki za wananchi wa kijiji chake kupitia uandishi wa makala na ushairi na kujikuta katika mfufulizo wa masaibu inayomfanya ajiulize mara mbili kuhusu mustakabli wa maisha yake binafsi, msichana ampendaye, wananchi wa kijiji chake na na taifa lake kiujumla.